

## Je Ninastahili Mpango wa Bima ya Taifa ya

## Ulemavu (NDIS) katika Australia ya Magharibi?

Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu katika Australia ya Magharibi unasaidia watu wenye ulemavu kupata huduma na msaada wanaohitaji. Mpango huu unasimamiwa Katika WA na Idara ya Jamii – Huduma za Walemavu (Department of Communities – Disability Services) (iliyojulikana hapo awali kama Tume la Huduma za Ulemavu – Disability Services Commission).

Wale wanaostahili pamoja na jamii zao au wanaowatunza watasaidiwa na Mratibu wa Mahali husika. Mratibu wa wa mahali atawahudumia kwa kuunda mpango unaotambulisha usaidizi ambao unaohitaji sasa na siku za baadaye. Watakusaidia kwa kukuunganisha na jamii, huduma zinazofadhiliwa na Serikali huduma za tawala ambazo zitakusaidia kufikia malengo yako. Mpango huu huangaliwa upya kila mwaka, au kulingana na vile malengo na mahitaji yako yanavyobadilika.

Ili kuweza kupokea msaada kupitia NDIS katika WA wewe au yule unayemhudumia mnahitaji kutimiza mahitaji ya miaka, Ukaaji nchini na Ulemavu au mahitaji ya kuingilia mapema.

Mahitaji ya kustahili kupokea msaada wa NDIS katika WA inajumuisha:

- ✓ Kuwa chini ya miaka 65 wakati wanapata msaada wa Ulemavu mara ya kwanza
- ✓ Kuwa Raiya wa Australia, au mkaazi nchini wa kudumu au visa Maalum ya Wamiliki ya (Aina ya, 444 – Raiya wa New Zealand ambao wanalindwa na visa maalum ya Wamiliki)
- ✓ Wanaishi kwa kudumu sehemu ambayo NDIS inatumika (unaweza kutembelea tovuti <http://www.disability.wa.gov.au/wa-ndis/wa-ndis/>)
- ✓ Vithibitisho vya ulemavu au ulemavu wa Maisha kupitia ripoti za kimatibabu kuonyesha kuwa wamegunduliwa na madhara kuonyesha kushidwa kufanya kazi za kila siku.

Watoto walemavu wa chini ya miaka 8 wanaweza kusaidiwa kupata msaada wa mapema. Kwa maelezo zaidi kuhusu kustahili msaada wa mapema tafadhali tembelea tovuti <http://www.disability.wa.gov.au/wa-ndis/wa-ndis/> au wasiliana na ofisi ya uratibu ya mitaa.

Kama huna uhakika kama unatimiza mahitaji ya kustahili msaada wasiliana na ofisi ya uratibu ya mitaa au pigia Chama cha Tawahudi (Autism Association) kwa nambari 08 9489 8900 kwa maelezo kwa jumla kuhusu NDIS katika WA.

*Tukiungwa Mkono na Idara ya Jamii (Huduma za Ulemavu)*